Jarida la Wizara ya Afya

# Afya Habari

JARIDA LA MTANDAONI LA WIZARA YA AFYA | TOLEO, NO. 21, JULAI 2024

TUNABORESHA AFYA
MTU NI AFYA • AFYA NI MTAJI



# TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA, JALI AFYA YAKO




## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. John Jingu
KATIBU MKUU

**MHARIRI**
Englibert Kayombo

**WAHARIRI WASAIDIZI**
Emmanuel Malegi
Atley Kuni

**WAJUMBE**
Englibert Kayombo
Emmanuel Malegi
Majid Abdulkarim
Said Nyaoza
Hassan Kimweri
Shaban Juma
Cletus Sanga
Abdulwaheed Madenge
Aisha Swahibu
Atley Kuni

**WASANIFU**
Englibert Kayombo
Said Nyaoza

@wizara_Afyatz
www.moh.go.tz

# YALIYOMO

Serikali kuendeleza mapinduzi sekta ya afya ....Uk 2





Katavi rrh yamkosha rais samia kwa usafi.... Uk 3

Mhe. Ummy ahimiza watumishi afya call centre 199 kuongeza Ufanisi kuhudumia wananchi..... Uk 4





Kanda ya magharibi kupata hospi-tali ya kanda .... Uk 5

Bima ya afya suluhisho la huduma bora za afya.... Uk 6





Wataalam kada za afya wafundishwe kuendana na Mahitaji ya nyakati.... Uk 6

Viongozi wa dini tumieni majukwaa yenu Kuhamasisha lishe bora...... Uk 7





# SERIKALI KUENDELEZA MAPINDUZI SEKTA YA AFYA

**Na. Majid Abdulkarim**
**KATAVI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali inaendeleza jitihada za kusogeza huduma za Afya karibu na wananchi kwa kuboresha miundombinu ya kutolea huduma kuanzia ngazi ya msingi ili kuimarisha huduma za Afya nchini.

Rais Samia amesema hayo Julai 14, 2024 Mkoani Katavi alipotembelea Hospitali ya Rufaa ya Mkoa huo ili kujionea hali ya utoaji wa huduma na maendeleo ya miradi ya ujenzi.
Rais Samia amesema Serikali tayari imeshapeleka fedha za ujenzi wa awamu ya pili ya Hospitali hiyo pia inatazamiwa kuongeza vifaa vya huduma za kibingwa.

“Hizi ni jitihada za Serikali kusogeza huduma za afya karibu sana na wananchi, ambapo ndani ya mkoa huu wa Katavi tumefanya kazi ya kuongeza vituo vya Afya, Hospitali za wilaya, kata hadi kule chini kwenye zahanati. Kwahiyo lengo ni kusogeza huduma za Afya karibu na Wananchi". Amesema Rais Samia na kuongeza. "Hospitali kama hizi tulizoea kuzisikia huko Dar es salaam Mwanza na Arusha lakini leo hospitali hii ipo Katavi, nimekwenda kuangalia Wodi ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati nimeona huduma iliyopo pale ni sawa na huduma iliyopo Dar es salaam Wodi ya watoto ambao hawakutimiza miezi 9, Mashine za kisasa na wataalamu wapo”. Amesisitiza Rais Samia.

Rais Samia ameongeza kuwa Serikali itaendelea kuimarisha Hospitali hiyo kwa ujenzi wa awamu ya pili na ya tatu kwa kujenga majengo mengine zaidi ya kutolea huduma.

“Kinachotumika sasa ni awamu ya kwanza ya Ujenzi wa hospitali hii lakini kuna awamu ya pili na awamu ya tatu kama inavyooneshwa kwenye ramani, fedha za ujenzi wa awamu ya pili tayari zimeshafika kwahiyo Hospitali hii itaendeleza ujenzi kujenga majengo mawili zaidi ya kutolea huduma na tutaendeleza ikamilike kama ilivyo kusudiwa kwenye Ramani”. Amefafanua Rais Samia.

Rais Samia pia ametumia fursa hiyo kuwasihi wananchi wa Mkoa wa Katavi na Tanzania kwa ujumla kujiunga na Mfuko wa bima ya Afya kwa wote.

“Niwaombe sana watakapokuja Mfuko wa bima kwa Afya, Kila Mwananchi anunue bima yake na familia yake mara moja kwa mwaka, unatibiwa na familia yako mwaka mzima. Tusaidieni kununua Bima za Afya ili tuweze kujenga na kutoa huduma zaidi katika mahospitali ya aina hii lakini hata hospitali zetu za mikoa na Wilaya na zile za kata kule chini, niwaombe sana twendeni tukaunge kono huduma hizi za Bima ya Afya ili Afya ya Mtanzania iweze kuimarika na kusambaa kwa kila mtanzania aweze kunufaika”. Amesema Rais Samia.

# KATAVI RRH YAMKOSHA RAIS SAMIA KWA USAFI

**Na. Majid Abdulkarim**
**KATAVI**

Rais wa Jamahuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amepongeza utendaji kazi wa Menejimeti ya Hospitali ya Rufaa ya mkoa wa Katavi kwa usafi uliopo Hospitalini hapo.
Akizungumza Julai 14,2024 wakati wa ziara yake ya ukaguzi wa Hospitali hiyo, Rais Samia amesema alichokiona katika Hospitali hiyo ni suala la kuigwa mfano kwa hospitali zingine nchini

"Ndugu zangu nimesimama kuelezea furaha yangu nimefika kukagua Hospitali na kuona inavyoendelea starehe yangu ni nilichokiona hapa ndani hakina tofauti na kilichopo kwenye Hospitali ni kubwa ambao nao kwa sasa wamejidhatiti juu ya suala la usafi muendele hivi hata kama ujenzi bado unaendelea,"amesema Rais Samia.

Amesema alipofika eneo hilo hakusikia harufu ya dawa hivyo amempongeza Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo Dkt. Serafin Patrice na Menejimenti yote ya Hospitali.

"Hospitali hii imenipa faraja wakati naongozwa kuangalia madaktari wote niliofuatana nao ni vijana ambao wangependa kuhudumu kwenye Miji mkubwa kama Dar es Salaam, Arusha au Mwanza lakini vijana wazalendo wamekubali kukaa Katavi na kuhudumia wananchi hongereni sana,"amepongeza Rais Samia.



Kuhusu fedha za ujenzi awamu ya pili, Rais Samia amesema zimefika na Hospitali hiyo itaendelea kujengwa majengo mengine zaidi ili kuhakikisha wananchi wa Katavi na mikoa ya jirani wananufaika na uwekezaji mkubwa wa serikali yao.

Rais Samia amesema Serikali ya awamu ya sita itaendelea kuzisogeza huduma za afya karibu na wananchi na utoaji wa huduma bora.

Amesema fedha zinazotumika kununua vifaa tiba ni nyingi ambapo lengo la Serikali kuhakikisha huduma bora za matibabu zinapatikana mpaka katika ngazi ya msingi mpaka Taifa.





# MHE. UMMY AHIMIZA WATUMISHI AFYA CALL CENTRE 199 KUONGEZA UFANISI KUHUDUMIA WANANCHI

**Na Aisha Swahibu,**
**DAR ES SALAAM**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu (Mb) amefanya ziara ya kikazi katika Kituo cha Kupokea na Kujibu hoja za Wananchi cha Wizara ya Afya (Afya Call Centre 199) kwa lengo la kufuatilia utendaji na ufanisi wa huduma zitolewazo kwa wananchi.

Akiwa kwenye ziara hiyo Julai 4, 2024 katika kituo hicho Mhe. Ummy Mwalimu amewapongeza watumishi wanaofanya kazi katika kituo hicho, akiwataka kuongeza juhudi na ufanisi katika kuhudumia wananchi na pia kuzingatia huduma bora kwa mteja, kutoa taarifa kwa usahihi na kwa wakati na kutumia muda kuwaelimisha wananchi wanaopiga simu kituoni hapo.

Aidha, Mhe Waziri Ummy pamoja na kukagua kazi zinazofanyika, alipata wasaa wa kufanya kikao na watumishi hao kusikiliza changamoto zao na maboresho ambayo wangependa yafanyike, utaratibu ambao Mhe Ummy amekuwa akifanya kwa Idara na vitengo mbalimbali ndani ya Wizara.

"Naibu Katibu Mkuu Dr Grace uko hapa, umeona na kusikia kazi kubwa inayofanyika katika kituo hiki na ongezeko la mahitaji ya rasilimali ikiwemo fedha, watumishi na vifaa, maagizo yangu kaeni na kituo hiki na kuja na mapendekezo ya namna bora ya kuboresha upatikanaji wa fedha, watumishi na rasilimali nyingine ili kuongeza ufanisi wa kituo hiki", alisema Mhe. Ummy.

Nae Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt.Grace Magembe amemuhakikishia Mhe Waziri kuwa maelekezo yake yatafanyiwa kazi kwa ukamilifu na tayari kuna baadhi ya maboresho yameanza kufanyika na kabla ya terehe 15/07/2024 kikao cha pamoja na watumishi hao kitafanyika.

Kituo hicho kinatoa taarifa mbalimbali kwa wananchi kwa njia ya simu na jumbe kwa lengo la kuelimisha umma ili kuwaepusha wananchi na tabia hatarishi zinazochangia kuongezeka na kuenea kwa magonjwa mablimbali ya kuambukiza na yasiyo ambukiza na pia wanapokea changamoto na pongezi zinazoelekezwa kwenye sekta ya afya kutoka kwa wananchi.

Akitoa taarifa mratibu wa kituo hicho Bi Beatrice Salanga amesema kwa siku wanapokea wastani kati ya Simu 2,000 hadi 3,000 kutoka maeneo mbalimbali na kuhakikisha wanapata ufumbuzi wa kila jambo kupitia Idara na vitengo mbalimbali vilivyoko chini ya Wizara ya Afya.

# KANDA YA MAGHARIBI KUPATA HOSPITALI YA KANDA

**Na Majid Abdulkarim**
**KIGOMA**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepanga kuanza ujenzi wa hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi wilaya ya Ujiji mkoani Kigoma.

Kauli hiyo imebainishwa na Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel wakati wa ziara ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philipo Mpango, mkoani Kigoma wakati alipotembelea eneo litakalo jengwa mradi ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Magharibi na Chuo cha Afya na Sayansi shirikishi Muhimbili (MUHAS) - Kampasi ya Kigoma
Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/25 imetenga kiasi cha fedha Sh. bilioni nne kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi hospitali hiyo ya Rufaa ya kanda Magharibi.

"Usanifu wa michoro ya ujenzi wa Hospitali hiyo ulianza February 2024 na sasa upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji ili ifikapo Julai 30, 2024 uwe umekamilika". amesema Dkt. Mollel
Akielezea eneo lililotengwa Mollel amesema Hekta 26.8 sawa na Ekari 66.2 ambazo zinapatikana Manispaa ya Kigoma Ujiji.


Ameongeza kuwa ujenzi wa hospitali hiyo unatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwezi Novemba, 2024 baada ya kazi ya ubunifu wa michoro na zabuni ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa awamu ya kwanza kukamilika.

Vilevile ameongeza kuwa awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi wa hospitali , kazi ya ubunifu na usanifu wa michoro inatekelezwa na Mshauri Elekezi, Kampuni Y&P Architects (T) Ltd kutoka Dar es salaam akishirikiana na Kampuni tanzu za Donmark (T) Limited kama wakadiriaji majenzi, Agreneb Consult Limited kama Wahandisi washauri wa umeme na mitambo, na Lomo Consult Limited kama Wahandisi miundo (Service Engineers).

Usanifu na ubunifu wa awamu ya kwanza ya mradi huo wa ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Magharibi - Kigoma unahusisha jengo la wagonjwa wa nje na huduma ya dharura-OPD/EMD Complex, Jengo la huduma za uchunguzi na utambuzi wa magonjwa -Diagnostic Service Complex.

Pia, eneo jingine ni ujenzi wa jengo la huduma za Dawa – Pharmaceutical Services Block, jengo la Upasuaji - Surgical Complex, jengo la Mama na Mtoto- Maternity Complex.

Lakini pia majengo mengine ni jengo la Wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu- Intensive Care Unit Block, jengo la utawala- Administration Complex, jengo la kutakasia vifaa tiba- Central Sterile Supply Department (CSSD), jengo la kufulia- Laundry, jengo la kuhifadhia Maiti- Mortuary, jengo la kuchomea taka hatarishi- Incinerator, uzio, njia za kupita wagonjwa na mazingira ya nje.



# BIMA YA AFYA SULUHISHO LA HUDUMA BORA ZA AFYA



**Na. Eglibert Kayombo**
**DAR ES SALAAM**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewataka watanzania kujiunga na huduma ya Bima ya afya kwa wote ili kuzidi kuimarisha huduma za Afya nchini

Pia Mhe. Rais amewataka wananchi wa Katavi kuuza mazao ili waweze kupata fedha na kujiunga na mfuko wa bima ya afya kwa wote.
Kauli hiyo ameitoa Julai 13, 2024 wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi wa Serikali wakati wa kilele cha wiki ya Jumuiya ya Wazazi ya Chama cha Mapinduzi kilichohitimishwa mkoani Katavi

Dkt. Samia amesema Serikali imeendelea kuweka misingi madhubiti ya vyanzo vya uhakika vya fedha ili kutekeleza bima ya afya kwa wote.

Amesema gharama za matibabu kwa sasa zimekuwa juu na suluhisho ni bima ya afya kwa wote.

"Niwaombe sana ndugu zangu wa Katavi unajua wakati mwingine umaskini ukiukumbatia na wenyewe unakukumbatia mnapouza mazao jitahidini kuhakikisha mnajiunga na bima ya afya kwa wote uweze ukatibiwa mwaka mzima bila usumbufu" amesema Mhe. Rais na kuongeza
"Tukifanya hivyo watanzania wote tutapata fursa ya kupata matibabu mazuri na ya viwango kulingana na uwekezaji mkubwa ulofanywa  na serikali yenu,"amesisitiza Dkt Samia





# WATAALAM KADA ZA AFYA WAFUNDISHWE KUENDANA NA MAHITAJI YA NYAKATI

**Na. Abdulwaheed Madenge**
**KIGOMA**

Katika kuendelea kuimarisha ubora wa huduma za Afya nchini, Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu amewataka wakufunzi wa vyuo vya Afya nchini kuhakikisha wanafundisha wanafunzi wa kada hiyo kufuatana na mabadiliko ya teknolojia na wakati ili waweze kuleta tija zaidi katika maendeleo ya sekta ya Afya kwa siku za usoni.

Mganga Mkuu amesema hayo Julai 16, 3024 mkoani Kigoma wakati alipotembelea kituo cha mafunzo ya maafisa wa kliniki na chuo cha mafunzo cha Kigoma Training College ambapo amesema Sekta ya Afya ni miongoni mwa sekta zenye mabadiliko ya kila siku hivyo ni vyema wanataaluma hao kuhakikisha wanakuja na taaluma ambazo zinakwenda na wakati na wanafunzi waweze kutoka na ujuzi wa kutosha.

Pof. Nagu amesema katika kulifanikisha hilo iko haja ya kuanza kwa kuwapa mafunzo, taaluma na ujuzi mpya mara kwa mara walimu wanaofundisha wataalamu hao.
"Walimu wanaofundisha hawa wataalamu wetu wapewe mafunzo kwa kuendana na mabadiliko ya wakati na pia wawe macho kuona mabadiliko na kutushauri tuongeze nini wapi ili hawa wataalamu watakao wapika waweze kuwa na tija kwa kuendana, kulingana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia na nyakati "Amesema Prof. Nagu.
Pia ameviasa vyuo vya Afya kuisaidia serikali kushughulikia uhaba wa wataalam kwa baadhi ya taaluma katika sekta hiyo hususani kwa kuja program zinaendana na mahitaji ya jamii.

"Hatuna wataalamu wa Radiolojia, wale wanaofundisha usikivu, tuna uhaba mkubwa wa wataalamu wa maabara, kwahiyo sekta hizi naomba mziangalie na pengine wala haziitaji miundombinu mikubwa sana, tusaidiane kuhakikisha wataalamu hawa." Amesema Prof. Nagu.
Prof. Nagu amesisitiza walimu kada za Afya pia kuhakikisha suala la maadili na nidhamu za watoa huduma linaimarika tangu vyuoni kwani ni nyenzo muhimu katika kuimarisha ubora wa huduma za Afya nchini.

Mganga Mkuu wa Serikali pia amepata fursa ya kutembelea vyuo vitakavyokuwa vinafundisha wataalam wa afya ngazi ya jamii, katika vyuo viwili vya Kituo cha Mafunzo ya Maafisa wa Kliniki (Kigoma COTC) na kigoma Training College kuridhika na Maandalizi.

# VIONGOZI WA DINI TUMIENI MAJUKWAA YENU KUHAMASISHA LISHE BORA

**Na Aisha Swahibu**
**DODOMA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya imewataka viongozi wa dini nchini kuendelea kutumia fursa ya majukwaa ya dini kuielimisha na kuiamasisha jamii juu ya masuala ya lishe na mtindo bora wa maisha ili kufikia adhma ya kuboresha Afya na ustawi wa Watanzania.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Msaidizi wa huduma za lishe Bi. Neema Joshua kutoka Wizara ya Afya akimwakilisha Mkurugenzi wa Kinga, Julai 18, 2024 jijini Dodoma wakati akifungua kikao cha kuhakiki na kupitisha maudhui ya jumbe yaliyopo kwenye rasimu ya mwongozo wa viongozi wa dini wa kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu masuala ya lishe nchini.

Bi. Neema amesema Wizara ya Afya inatambua nafasi na ushawishi mkubwa wa viongozi wa dini katika jamii, hivyo Wizara itaendelea kushirikia na viongozi wa dini kufanikisha adhima hiyo kwa kuandaa mwongozo utakaotumika kutoa elimu na hamasa ya masuala ya Lishe kupitia majukwaa ya dini katika jamii.

“Tunategemea michango yenu yenye tija itakayosaidia kuhakikisha mwongozo huu unakuwa na maudhui yanayokidhi mahitaji ya jamii yetu, ushirikiano wenu katika hatua hii ni muhimu sana na tunaomba muendelee kutuunga mkono kwenye safari hii ya kuboresha afya na ustawi wa jamii zetu kupitia kuelimisha na kuhamasisha masuala ya lishe kwa Watanzania”. Ameeleza Bi. Neema.

Aidha, ameeleza kuwa Tanzania inakabiliwa na changamoto ya utapiamlo ikiwemo lishe pungufu, upungufu wa vitamini, madini na lishe ya kuzidi hivyo serikali inaendelea kuweka mikakati ya kupambana na lishe duni kwa jamii.

“Takwimu za mwaka 2022 zinaonesha kuwa asilimia 30 (watoto 3 kati ya 10) walio na umri chini ya miaka mitano wamedumaa, asilimia 12 (mtoto 1 kati ya 10) walio na umri chini ya miaka mitano wana uzito pungufu hali inayoweza kusababisha magonjwa ya mara kwa mara, athari mbaya za ukuaji na ustawi wao kwa ujumla. Watoto wenye utapiamlo hawakui ipasavyo kimwili, kiakili na kisaikolojia na huwa na uwezo mdogo wa kufaulu masomo yao shuleni”. Ameeleza

Kwa upande wake Askofu Joseph Mpalagu amesema ili kuongoza waumini katika ibada ni lazima kuongoza waumini wenye Afya bora na kuahidi kuutumia muongozo huo katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu lishe bora ili kufikia lengo la Pamoja la kuwa na jamii yenye Afya bora.

"Kwenye maandiko ya Mungu biblia inasema miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu hivyo miili yetu ni sehemu ya kufanyia ibada hivyo inahitajika kuwa ni miili yenye afya nzuri, akili yenye ubunifu mzuri kwa ajili ya huduma za kiroho, hivyo baada ya kupitishwa kwa muongozo huu tunaahidi kwenda kuwafundisha waumini wetu”.





# BILIONI TANO ZATOLEWA KUGHARAMIA HUDUMA ZA UBINGWA BOBEZI KWA WENYE UHITAJI

**Na Hassan Kimweri**
**DAR ES SALAAM**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa kiasi cha shilingi Bilioni 5 kwa mwaka wa fedha 2023/24 ili kusaidia kugharamia upatikanaji na utoaji wa huduma za matibabu ya Ubingwa na Ubingwa Bobezi kwa wananchi wenye uhitaji kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete.

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu ameyasema hayo Julai 19, 2024 alipotembelea Hospitali ya Taifa MUHIMBILI kwa lengo la kuangalia huduma mbalibali zinazotolewa za kibingwa na ubobezi kupitia fedha zilizotolewa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

"Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anaendelea kuhakikisha wananchi wasiokuwa na uwezo wakumudu gharama kubwa za matibabu ya Ubingwa na Ubingwa bobezi na wenye uhitaji wanapata huduma hizo." Amesema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy amesema kiasi cha Shilingi Bilioni 2.6 zimetolewa kwa Hospitali ya Taifa Muhimbili ambapo awamu ya kwanza zimegharamia wagonjwa wa kupandikiza Figo (wagonjwa 6); kupandikiza vifaa vya kusaidia kusikia kwa watoto 10, kupandikiza ULOTO kwa wagonjwa 5 pamoja na kusaidia watoto 10 wenye matatizo ya mfumo wa Ulolojia.

Kwa upande wao, wanufaika wa huduma hizo, kwa pamoja wameiomba Serikali kushusha huduma hizo za Ubingwa Bobezi ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa ambapo kuna wananchi wengi ambao pia wanahitaji huduma hizo.

Waziri Ummy ameahidi kulifanyia kazi jambo hilo kwa kuona ni hatua gani za awali za Ubingwa Bobezi zinaweza kuanza kutolewa katika ngazi hizo ili kila Mtanzania aweze kunufaika na huduma hizo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili amemuhakikishia Waziri wa Afya kuwa Hospitali hiyo itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma bora kwa wananchi na kutekeleza Sera, Miongozo na Maelekezo ya Serikali katika kuwahudumia wananchi wanaopata huduma katika vituo Viwili vya Upanga na Mloganzila.

# TUMIENI MAJUKWAA YA MICHEZO KUIMARISHA AFYA



**Na Abdulwaheed Madenge**
**DODOMA**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa ameiagiza Wizara ya Afya kuendelea kushirikiana na wadau wanaoandaa michezo ya riadha na mengineyo kwa lengo la kutumia majukwaa hayo kufikisha elimu ya afya kwa umma na kubali mitindo ya maisha inayochochea ongezeko la Magonjwa yasiyoambukiza.

Waziri Mkuu Majaliwa ametoa wito huo Julai 28, 2024 wakati akihitimisha mbio za NBC Marathon iliyokuwa na lengo lakuchangia huduma za afya pamoja na kuimarisha afya kwa njia ya mazoezi.

"Wizara ya Afya endeleeni kushirikiana na wadau wote wa michezo wanaondaa michezo hii inayotuleta wote kwa pamoja kwa lengo lakufikisha elimu ya umuhimu wa kufanya mazoezi kama ambavyo leo tulivyofanya" Amesema Majaliwa

Waziri Mkuu Majaliwa ameongeza kuwa kwa mujibu wa taarifa mbali mbali Wizara ya Afya zinaonyesha kwa siku za karibuni Magonjwa yasiyo ambukiza yameongezeka tofauti na hali ilivyokuwa huko nyuma na hususani ni Magonjwa ya kisukari, sinikizo la damu, Moyo na Figo.

"Kwenye eneo hili ni muhimu tuendelee kupokea ushauri wa wataalam wa afya, kukaa bwete ni kukaribisha magonjwa hayo yasiyoambukizwa ni muhimu kushiriki katika michezo mbalimbali na mimi naamini sote tumeanza kujali kwa kuzingatia kufanya Mazoezi" amesema Waziri Mkuu Majaliwa.

Waziri Mkuu ametumia wasaa huo kuishukuru Benki ys NBC kwa niaba ya watanzania kwa kuendelea kushirikina na Serikali kuchangia na kuwezesha uboreshaji wa sekta ya Afya kwa maeneo yanayogusa Ustawi wa jamii.

"Mbio hizi zimekusanya michango mbalimbali kwa lengo la kuisaidia Sekta ya Afya, NBC mmendelea kutuonyesha njia kwa ubunigu wenu wa kukusanya Fedha kwa ajili ya kuwekeza kwenye Sekta ya Afya, Fedha ambayo ameitaja Mkurugenzi Mkuu Millioni 300 ambayo itakabidhiwa leo ni kwa lengo ya kuusaidia mapambano dhidi ya Kansa ya Mlango wa shingo ya kizazi kwa wanawake ambayo itakabidhiwa kwa Taasisi ya Kansa ya Ocean Road,



# WATAALAM WA AFYA TUMIENI TAKWIMU KUCHECHEMUA UBORA WA HUDUMA

**Na Abdulwaheed Madenge**
**KIGOMA**

Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu amewataka wataalamu wa Afya nchini kutumia takwimu na tafiti mbalimbali kama kiongozo cha kusaidia kutambua na kutatua chagamoto zinazoikabili sekta ya Afya katika maeneo yao ya kiutendaji ili kufikia lengo la Serikali la kuimarisha zaidi ubora wa huduma za Afya nchini.

Prof. Nagu amesema hayo Julai 18, 2024 wakati akiendelea na ziara yake Mkoani Kigoma katika Wilaya ya Buhigwe ambapo ametembelea Hospitali ya Wilaya hiyo kujionea hali ya utoaji wa huduma za Afya na ujenzi wa miradi ya maendeleo.
Prof. Nagu amesema bila kutumia takwimu haitawezekana kujua changamoto jambo litakalopelekea ugumu pia katika kutatua changamoto na kuboresha hali ya utoaji wa huduma za afya nchini.

Amesema kupitia takwimu ameona jinsi wilaya hiyo ilivyojifanyia tathimini na kujifanyia maboresho katika kudhibiti vifo vya wakina mama wajawazito na watoto wachanga vitokanavyo na uzazi ambapo awali 2021 vilikuwa vifo 7 vya wakina mama wakati kwa mwaka huu mpaka sasa ni Kimoja pekee na kwa upande wa watoto wachanga vilikuwa vifo 48 na sasa ni vifo 12 pekee

Prof. Nagu amepongeza pia Wilaya ya Buhigwe kwa kuimarisha mapambano dhidi ya magonjwa ya mlipuko maeneo ya mpakani licha ya kuwa na eneo kubwa la mpaka.

“Pamoja na kuwa mna eneo la mpaka kubwa lakini niwapongeze mpaka sasa hakuna magojwa ya mlipoko hakuna Surua, Kipindupindu na mengineyo pamoja ya kwamba apa tunajua ni mpakani na mpaka mkubwa wa Burundi, kwasababu naangalia changamoto na mnazifanyia kazi na mnatatua, hii ni mfano wa kutumia takwimu kufanya maamuzi “Amesema Prof. Nagu

Awali akisoma taarifa ya hospitali ya Wilaya ya Buhigwe Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo Dkt. Baraka Kemero amesema Halmashauri hiyo ilipokea Fedha Tsh. million 800 kwa ajili ya kujenga majengo ya wodi ya Wanaume, wodi ya wanawake na wodi ya watoto, jengo la kuhifadhia maiti ambapo ujenzi wa wodi hizo umekamilika kwa asilimia zaidi ya 90 na unatarajia kuwanufaisha zaidi ya wananchi 254,342.

Kwa upande wake Mgaanga Mkuu wa Wilaya ya Buhigwe, Dkt. Innocent Mhagama amesema Kukamilika kwa mradi huo kutasaidia kupanua huduma za afya zilizoboreshwa kwa wakazi wa Wilaya ya Buhigwe na kuvutia watu kutoka nchi jirani Pia utasaidia kupunguza adha kwa wanabuhighwe kwenda hospitali za mbali, kupunguza gharama za matibabu na vifo.

# UELEWA MDOGO CHANZO CHA UTAPIA MLO KWA JAMII

**Na Emmanuel Malegi**
**DAR ES SALAAM**

Uelewa mdogo wa jamii kuhusu masuala ya lishe ikiwemo matumizi sahihi ya vyakula vinavyopatikana katika maeneo mbalimbali ya nchi ni miongoni mwa sababu zitajwa kuchangamoto utapiamlo ndani ya jamii.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma Lishe Wizara ya Afya Bi. Neema Joshua Julai 23, 2024 jijini Dar Es Salaam wakati akizungumza na Viongozi wa Kanisa la Waadventista wa Sabato Jimbo kuu la Kusini mwa Tanzania, ikiwa ni muendelezo wa vikao vya kuhakiki na kupitisha maudhui ya jumbe zilizopo kwenye rasimu ya mwongozo wa viongozi wa dini wa uhamasishaji na uelimishaji jamii juu ya masuala ya lishe nchini.

Bi. Neema amesema ili kuondoa changamoto ya utapiamlo kwa nchi Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kushirikiana na Viongozi wa dini ili kuhakikisha elimu na uhamasishaji wa lishe bora unawafikia watanzania waliowengi.

“Lishe bora ni msingi wa ustawi mzima wa maisha ya binadamu katika nyanja zote za Maisha, nidhahiri kuwa, afya njema ambayo kwa kiasi kikubwa huchagiwa na Lishe bora, humwezesha mtu kutimiza majukumu yake ya kila siku kwa ufanisi ikiwemo kushiriki katika ibada, sala, kutafakari pamoja na kufanya kazi kwa tija kwa maendeleo yake binafsi, jamii na Taifa kwa ujumla" amesema Neema na kuongeza.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Kanisa la Waadventista wa Sabato Jimbo kuu la Kusini mwa Tanzania, Mchungaji Dkt. Jeremiah Izungo amesema ameishukuru Wizara ya Afya kwa maono yake ya kuona umuhimu wa Viongozi wa dini kushirikishwa kwenye masuala ya lishe jambo ambalo linawapa nguvu ya ziada viongozi wa dini kulisemea kwa waumini wao.

Katika hatua nyingine amesema mwili wa binadamu ni hekalu la mungu na ni mali yake hivyo changuo ya namna ya kula na nini chakula ni lazima kizingatia mratibu wa mwili ambae ni Mungu, kufanya vinginevyo ni kumkosea na kukatisha maisha ya mwanadamu.

“Ili tuwe salama tunapaswa kuupende huu mwili sawa sawa na mapenzi ya mwenye mwili na sio vinginevyo[1], “Basi mlapo au mnywapo au mtendapo neno lolote fanyeni yote kwa utukufu wa mungu”; 1 Wakorintho 10;31” amesema Mch. Dkt. Izungo.



# IMARISHENI MIFUMO YA TAARIFA KUDHIBITI MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA



**Na Atley Kuni**
**DODOMA**

Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu amewataka waratibu wa mikoa wa Magonjwa yasiyoambukiza kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa taarifa na rejesta za magonjwa kwa ajili kusaidia kufanya maamuzi sahihi.

Prof. Nagu, amesema hayo Julai 25, 2024 wakati akihitimisha kikao cha waratibu wa mikoa wa magonjwa yasiyoambukiza kilichofanyika mkoani Dodoma.

“Nilishatoa maelekezo ya kuanzishwa kwa rejesta za magonjwa yasiyoambukiza pamoja na kuboresha mifumo ya ukusanyaji taarifa kwenye ngazi zote, ninafurahi kuona katika ngazi ya msingi huduma na rejesta za magojwa ya kisukari na shinikizo la juu la damu imefanyiwa kazi, bado magonjwa mengine ambayo bado yanasumbua jamii, amesema Prof. Nagu na kuongeza

"Napenda kuwakumbusha kuhusu masuala ya kuimarisha mifumo na ukusanyaji wa taarifa kwaajili ya kusaidia ukufanya maamuzi sahii kwenye maeneo yetu," amefafanua Prof. Nagu.

Mganga Mkuu huyo wa Serikali ametilia mkazo suala la ubora wa huduma kwenye magonjwa yasiyoambukiza na kupewa kipaumbele kwakua wameshuhudiwa ongezeko la watu wenye matokeo hasi ambayo yangeweza kuzuilika endapo watoa huduma wangesimamia ubora wa huduma zinazotolewa.

“Tunajukumu la kufanya kwenye kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa, nitoe rai tukasimamie ubora wa huduma kwa kutumia vigezo sahihi, aidha nikutale Mkurugenzi wa Tiba na timu yako pamoja na Mkurugenzi wa Afya, ustawi na lishe kuhakikisha suala la ubora wa huduma linafatiliwa kwa karibu” ameagiza Prof. Nagu.

Wakati huo huo Prof. Nagu ametala jamii ipatiwe elimu sahihi ya magonjwa yasio yakuambukiza na hususani ni maeneo yenye changamoto zaidi" Amesema Prof. Nagu.
Prof. Nagu ametumia fursa hiyo kutaka ushirikiano kati ya sekta za elimu, kilimo, mazingira na ili kufikia malengo kwa haraka na ufanisi mkubwa.

Tathmini ya ubora wa huduma za MYA kwa kutumia mfumo wa ubora wa huduma za kisukari kwa kuangalia kiwango cha udhibiti wa sukari kwenye damu cha HbA1c imebainika kuwa ni asilimia 22 yaani watu 2 kati ya watu 10 ndio udhibiti wao wa sukari kwa miezi mitatu inafikia kiwango cha kuridhisha.



# LISHE DUNI NI VITA YA PAMOJA

**Na Aisha Swahibu**
**DAR ES SALAAM**

Serikali imesema suala la lishe duni chini ni vita yenye athari kubwa kwa taifa huku ikiwataka wadau na viongozi wa dini kuunganisha nguvu kukabiliana nayo.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Lishe Wizara ya Afya, Bi. Neema Jushua, Julai 24, 2024 jijini Dar Es Salaam wakati akizungumza na viongozi wa Baraza la Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), ikiwa ni muendelezo wa vikao kazi vya kuhakiki na kupitisha maudhui ya jumbe zilizomo kwenye rasimu ya mwongozo wa viongozi wa dini wa uhamasishaji na elimishaji jamii kuhusu masuala ya lishe nchini.

Bi. Neema amesema lishe ina wigo mpana sana kwenye maendeleo ya taifa.

"Hali ya lishe ya nchi yetu imeharibika na lishe mbovu na hili linaweza kutishia usalama wa nchi kwa kuwa watu wake hawazingatii milo sahihi na mitindo bora ya maisha yao. Endapo watu hawana uwezo wa kufikiri sawa sawa kwa kujitengenezea wenyewe na kutegemea kutoka nje, hali hii inaweza kuathiri usalama wa nchi."

Awali, akimkaribisha Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Lishe kutoka Wizara ya Afya, Bw. Japhet Msoga amesema lengo la kikao hicho ni kupitisha maudhui ya ujumbe yaliyomo kwenye rasimu ya mongozo kwa ajili ya matumizina viongozi wa dini na kuwasilisha nadharia ya lishe kwa viongozi wa dini kwa ajili ya kujenga uelewa kuhusu masuala ya lishe.

"Lengo ni kuendeleza ushirikiano kati ya viongozi wa dini na Wizara ya Afya kwenye juhudi za kuboresha hali ya lishe nchini ambapo matarajio ya Wizara ya Afya ni kupata Mwongozo wa Viongozi wa Dini wa Uhamasishaji na Uelimishaji Jamii kuhusu masuala ya lishe nchini."




# MARUFUKU KUTOA KADI ZA HOMA YA MANJANO KIMAGENDO BILA KUCHANJA

**Na Abdulwaheed Madenge**
**KIGOMA**

Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu amekemea na kulaani vikali Tabia ya baadhi ya watoa huduma za Afya mipakani wasio waadilifu kuuza au kutoa kadi za homa za manjano kwa magendo kwa watu ambao hawajachanjwa.

Prof. Nagu amesema hayo Julai 16, 2024 wakati wa ziara yake Mkoani Kigoma ambapo ametembelea bandari ya Kibirizi na bandari ya Kigoma na kujionea namna Maafisa Afya wamejipanga kudhibiti magonjwa ya mlipuko mipakani ambapo amesema Serikali itawachukulia hatua kali wale wote watakaobainika kwenda kinyume na agizo hilo.

"Tusiuze kadi za homa ya manjano kimagendo bila kuchanja, utaratibu upo kuna nchi zimeorodheshwa na mtu akisafiri akitoka katika nchi hizo lazima awe amechanjwa na kuchanjwa maana yake aoneshe uthibitisho wa kadi, sasa kuna wengine wanaingia hawana hizo kadi wanauziwa bila kuchanjwa sio kigoma peke yake naongelea bandari zote tuwe waaminifu katika kutenda kazi zetu, tufuuate taratibu na miongozo kwamba tusitoe kadi za homa ya manjano bila kuchanja" Amesema Prof. Nagu.

Pia Prof. Nagu amewataka wataalam wa afya wa mipaka na bandarini kutambua ukubwa wa jukumu ambalo wamepewa na Serikali katika kuhakikisha nchi yetu inabaki salama.

"Tunajukumu kubwa sana lakuhakikisha watu wenye magonjwa ya kuambukiza hawaingii nchini kwetu, na pia tulinde mipaka yetu dhidi ya dawa ambazo sio Sahihi au Feki lakini pia na vifaa tiba, Tunawategemea ninyi sana kuhakikisha mnailinda mipaka yetu"

Aidha Prof. Nagu ameishukuru Mamlaka ya Bandari Tanzania TPA kwa kuendela kutoa ushirkiano kwa Wizara ya Afya hasa katika maeneo hayo jambo linalosaidia kuimarisha usalama wa nchi yetu

"Tushirikiane kudhibiti magonjwa na vifaa tiba, Vilivyo vibovu visiingie nchini kwetu lakini pia na sisi kuzuia vitu na madawa yetu kutoroshwa, kwahiyo naomba sana tushirikiane tuendelee kudhibiti tusipate magonjwa ya Mlipuko, dawa zisizo salama, vitendanishi na Dawa ambazo hazina ubora" Amesema Prof. Nagu.

# MAFUNZO YA KIROHO YANAHITAJI MIILI YENYE AFYA BORA

**Na Cletus Sanga**
**DAR ES SALAAM**

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Afya wa Wizara ya Afya Bi. Neema Joshua amesema masuala ya kiroho na kiimani yanabebwa na mwili kuwa na afya bora na utimamu wa akili.

Bi. Neema amesema hayo Julai 22, 2024 na wakati wa kikao kazi na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) jijini Dar Es Salaam, ikiwa ni muendelezo wa vikao vya uhakiki na kupitisha maudhui ya jumbe yaliyopo kwenye rasimu ya mwongozo wa viongozi wa dini kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya masuala ya lishe nchini.

Amesema Wizara ya Afya inatambua ushirikiano uliopo baina ya viongozi wa dini kuhusu ya masuala ya Afya ikiwa ni moja ya juhudi zinazofanywa ambazo zimeleta mafanikio ya makubwa kwa kuwafikia watu wengi zaidi.

“Wizara ya Afya imeona Viongozi wa dini wana wafuasi wengi na wanaaminika kwa jamii pia wana mkono mrefu kuliko Serikali kwa sababu wanawafikia watu wengi, hivyo mkakati wa kuwatumia viongozi wa dini pamoja na kushirikiana nao kwenye kuhamashisha na kutoa elimu juu ya masuala ya lishe bora kwa jamii hivyo tunatamani uwe endelevu ili kuhakikisha tunakuwa na jamii yenye afya bora”. Amesema Bi. Neema.
Mkurugenzi huyo amebainisha kuwa viongozi wa dini ndio wametumika toka kuanza kwa kuandaa muongozo huu hadi hivi sasa unapoelekea utekelezaji, na kuimarisha ushirikiano ili kuhakikisha kile kilicholengwa kiwafikie kweli wananchi.

Awali Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania, Padri Dkt. Charles Kitima amesema dawa kubwa kuliko zote katika mwili wa binadamu ni lishe hivyo ameihakikishia wizara ya afya kuwa kwa kutumia jumuiya zao wanawafikia watu wengi na kueleza kuwa mtandao wa jumuiya za katoliki uko wazi hivyo wizara iwe huru kuwatumia ili kuifikia jamii.



# DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050 BIMA YA AFYA KWA WOTE ITAKUWA CHACHU KUBOREHA HUDUMA ZA AFYA: MHE.

**Na. Atley Kuni**
**DAR ES SALAAM**

Waziri wa Afya Mhe.Ummy Mwalimu ameiasa tume inayopokea maoni kuhusu maandalizi ya Dira ya Taifa 2050 suala la Bima ya Afya kwa wote liwe kipaumbele ili kuzidi kuboresha huduma za Afya.

Mhe. Ummy amesema kote ulimwenguni gumzo kwa sasa ni Afya kwa wote hivyo Tanzania kama nchi hatunabudi kuingiza suala la Bima ya Afya kwa wote katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050.

Mhe. Ummy ameyasema hayo Julai 06, 2024 wakati wa Kongamano la kitaifa la wadau wa Sekta ya Afya kuhusu maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

"Ndugu zangu watanzania kama kila mmoja wetu akiguswa na kuchangia huduma za Bima ya Afya ni dhahiri shahiri kuwa huduma zetu zitaboreka" amesema Waziri Ummy.

"Tusingoje mgonjwa yupo, Muhimbili, JKCI, Bugando au mahala pengine ndio uanze kukimbizana na Bima ya Afya, hakuna Bima ya hivyo, tuzingatie miongozo na Sheria inavyotaka" amesema Mhe.Ummy

Katika hatua nyingine Waziri Ummy amesema, Wizara ya Afya imefanya vizuri katika Dira ya 2000/2025 inayomaliza muda wake katika masuala kadhaa mbali ya kukabiliwa na baadhi ya magonjwa ya mlipuko kama Kovidi 2019.

"Tumefanikiwa sana, juu ya suala la wanawake kujifungulia katika Vituo vya Afya, kwani imeongezeka kutoka asilimia 41 mwaka 2000 hadi kufikia asilimia 81 kwa sasa na tutajitahidi ifikapo 2025 tuwe tumefikia asilimia 100". amesema Mhe. Ummy

Akifungua Kongamano hilo lililowashirikisha wadau wa Afya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji Mhe. Prof. Kitila Mkumbo ameipongeza Wizara ya Afya kwa kuandaa Kongamano hilo ikiwa ni wizara ya kwanza kufanya hivyo.

"Ninyi ndio mnao ijua Sekta ya Afya, mmeamua kuwaita wadau wenu waje watoe maoni yao, ili sisi iwe kazi yetu iwe rahisi, tunapo andaa Dira ya Taifa ya 2050" Amesema Prof. Kitila

Akitoa Salaam za Ofisi ya Rais TAMISEMI Naibu Waziri Dkt. Festo Dugange, ameiomba kamati inayopokea maoni kuzingatia suala la kuboresha huduma za Kibingwa katika ngazi ya msingi.





# RRH. SIMAMIENI VITUO VILIVYO CHINI YENU

**Na Abdulwaheed Madenge**
**DODOMA**

Mkurugenzi wa Idara ya Tiba Dkt. Hemed Nyembea amesema mifumo ya Afya nchini inazitambua Hopitali za rufaa za mikoa kuwa kiunganishi kati ya huduma za afya ngazi ya msingi kwa kuwa na jukumu la kuhudumia vituo vya afya ngazi zote za mkoa.

Ameyasema hayo Julai 4, 2024 jijini Dodoma wakati wa zoezi la ukaguzi shirikishi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma ambapo kamati ya ukaguzi kutoka wizara ya afya ilitembelea na kukagua idara hospitalini hapo.

Amesema dhana hiyo inaipa jukumu hospitali za mikoa kuhudumia vituo vya afya ngazi za chini ili vituo hivyo viwe na uwezo wa kuhudumia wagonjwa kwa kiwango chao na kupunguza rufaa za wagonjwa kwa hospitali za mikoa.

“Hospitali ya rufaa ya mkoa inatakiwa kufanya huduma za mkoa (outreach) kwenye Halmashauri za Mkoa, ambapo nimeambiwa hapa zinafanyika hivyo ninahimiza kuendelea kupanga ratiba vizuri ili kila idara iweze kutembelea kila Halmashauri ya mkoa kwa kufuata taarifa juu ya changamoto wanalizonazo na kutatua changamoto hizo,”. Amesema Dkt. Nyembea

Dkt. Nyembea ameitaka menejimenti ya Hospitali hiyo kuelewa vizuri dhana ya ubora wa huduma kwa kuifahamu misingi yake na kuiwakilisha kwa kila mtumishi wa kila idara na kuongeza kuwa suala la huduma kwa mteja linapaswa kubeba na kuchukuliwa kwa uzito na kila mtumishi wa sekta ya afya.

“Malalamiko mengi yanayokuja yanaonyesha kuwa suala la mawasiliano limekuwa ni shida ambapo mawasiliano ni sehemu muhimu ya kumhudumia mgonjwa, tunafahamu wote na tumesoma kuwa mgonjwa kwenye matibabu ndio kiini cha ugonjwa alio nao na kufanya maamuzi, tujitahidi sana kuboresha huduma kwa mteja “. Ameeleza.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma Dkt. Ernest Ibenzi amesema Hospitali hiyo imeendelea kuunga mkono juhudu za Serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kuhakikisha watanzania wanapata huduma bora na kuwafikia walipo kwa kupeleka Madaktari bingwa maeneo mbali mbali ya nchi kwa lengo la kusaidia utoaji wa huduma sambamba na kusambaza vifaa tiba kwa wagonjwa waliovunjika mifupa mirefu.

“Juzi tulipeleka madaktari bingwa 12 katika kambi ya matibabu mkoani Arusha kwa ajili ya kusaidia kutoa huduma na pia hospitali tunasambaza vifaa tiba vya kutibu wagonjwa waliovunjika mifupa mirefu ambapo tayari tushapeleka Hospitali ya Mt. Meru, Njombe, Shinyanga na hivi sasa tunaelekea Morogoro lengo likiwa ni huduma hizi za mifupa zifanyike katika hospitali zote za mikoa”

# UTARATIBU MPYA WA UPIMAJI WA VVU KUONGEZA WIGO KWA WAPIMAJI

**Na Said Nyaoza**
**DAR ES SALAAM**

Utaratibu mpya wa kitaifa wa upimaji wa Virusi vya UKIMWI kwa vipimo vitatu ili kuthibisha kuwa mtu ana maambukizi ya VVU utasaidia kuongeza wigo wa upimaji wa VVU nchini.

Hayo ameyasema Kaimu Meneja Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini Dkt. Ona Machangu Julai 02, 2024 Jijini Dar es Salaam katika ufunguzi wa kikao cha kutambulisha mwongozo mpya (Algorithim) ya kitaifa kuhusu upimaji wa Virusi vya UKIMWI, ambapo mtu atapimwa ama kujipima na kugundulika kuwa na virusi vya UKIMWI kwa kipimo cha awali atalazimika kupima vipimo vingine viwili vya uhakiki ili kuthibisha kuwa anamaambukizi ya VVU.

Dkt. Machangu amesema Lengo mahususi la kutumia vipimo vitatu ni kuhakikisha wigo wa upimaji unaongezeka kwa kupima vipimo ambavyo vitaleta majibu sahihi zaidi ili kuleta manufaa na kusaidia huduma za uchunguzi kwa watu ili waweze kushawishika kupima na kuanza dozi mara moja endapo watagundulika.

Pia Dkt. Machangu amesema ili kufikia lengo la kutokomeza maambukizi mapya ya UKIMWI mwaka 2030, Wizara ya Afya inalenga kuendelea kuboresha huduma za upimaji lli kuhakikisha kila mtu anafikiwa na huduma za upimaji na kujua hali yake ya kiafya.

"Tanzania tupo katika malengo ya kidunia ya 95 na kutokana na tafiti za viashiria zinaonesha 95 ya kwanza ya upimaji kama nchi tupo asilimia 83 hivyo tunalengo hasa la kuhakikisha tunamfikia kila mtu na huduma za upimaji nchini"

Aidha Dkt. Machangu amewasihi wananchi kuendelea kujitokeza kupima afya zao ili kutambua hali zao za kiafya na kuanza dozi ya kupunguza makali ya VVU mara moja
"Niwakaribishe watanzania kufika kwenye vituo vya afya kupata huduma za upimaji pia kuna huduma za kujipima kwani ni vizuri kujua afya yako ili kufurahia maisha". Amesema Dkt. Machangu.

Kwa upande wake Mwakilishi kutoka shirika la Afya Duniani (WHO) Bi. Maria Kelly amesema kama wadau wa maendeleo wamejidhatiti kwa kuendelea kusaidiana na Serikali ili kuhakikisha mpango huo wa upimaji unaweza kutekelezeka.





# WADAU WAASWA KUCHANGIA MFUKO WA BIMA YA AFYA KWA WOTE

**Na. Abdulwaheed Madenge**
**DAR ES SALAAM**

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu amewaomba wadau wa Maendeleo ndani ya sekta ya Afya kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali hususani kipindi hiki cha kuelekea kwenye utekelezaji wa mpango wa Bima ya Afya kwa wote nchini.

Dkt. Jingu ametoa wito huo Julai Mosi, 2024 jijini Dar Es Salaam wakati wa kikao kazi cha kuridhia mpango kazi na matumizi ya fedha zinazotolewa kupitia mfuko wa pamoja wa afya zikiwemo Balozi, na Benki ya Dunia kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Dkt. Jingu amesema sheria ya Bima ya Afya kwa wote iliyosainiwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan inalengo la kuona kila Mtanzania anapata huduma bora za Afya muda wote hasa kwa makundi maalum wakiwemo wakinamama wajawazito, watoto walio na umri chini ya miaka mitano na wananchi wasio na uwezo.

“Wadau wa sekta ya Afya wamekuwa wakiunga mkono juhudi za serikali kwa kuchangia kupitia mfuko wa afya ya jamii(CHF) na kuimarisha huduma za afya nchini, hivyo niwaombe kuendelea kuunga mkono utekelezaji wa mpango wa Bima ya Afya kwa wote utakao kuwa mkombozi kwa wananchi wasio na uwezo” Dkt. Jingu amesema.
Aidha, Dkt. Jingu amewashukuru wadau kwa kuendelea kuchangia bajeti ya wizara ya afya ambayo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kwa kipindi cha miaka 3 iyopita.

Awali akimkaribisha Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu, Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu alisema Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kuimarisha ubora wa huduma za afya na kusogeza karibu na Wananchi hadi katika ngazi za msingi.

“Kwa sasa kila mtanzania anapata huduma bora za afya kwani tumepeleka madaktari bingwa na ubingwa bobezi kwenye hospitali za wilaya ambapo mbali ya kutoa huduma kwa wananchi pia wamewajengea uwezo na ujuzi kwa watumishi wa afya katika hospitali hizo” Amesema Prof. Nagu



# BILIONI 145 KUCHANGWA NA WADAU, MFUKO WA AFYA WA PAMOJA

**Na Abdulwaheed Madenge**
**DODOMA**

Serikali kupitia Wizara ya Afya inatarajia kupokea bilioni 145 kwa mwaka wa fedha 2024/25 kutoka bilioni 126 mwaka 2023/24 ongezeko la asilimia 15, kutoka kwa wadau wanaochangia sekta ya afya kupitia mfuko wa afya wa pamoja (Health Basket Fund)

Hayo yamesemwa Julai Mosi, 2024 na Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu wakati wa kikao kazi cha kuridhia mpango kazi na matumizi ya fedha zinazotolewa kupitia mfuko wa pamoja wa afya zikiwemo Balozi na Benki ya Dunia kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Dkt. Jingu amesema kati ya fedha hizo shilingi bilioni 130.1 zitagawanywa kwenye Halmashauri, bilioni 5.9 Wizara ya Afya , bilioni 5.9 Mikoa na bilioni 2.9 zitakwenda Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Aidha, ameongeza kuwa lengo la Mchango wa mfuko wa afya wa pamoja kutoka kwa wadau hao ni kuimarisha Huduma za Afya katika ngazi ya msingi hususani kwenye ununuzi wa vifaa tiba, dawa na kuimarisha huduma za Chanjo.

"Mbali na maeneo hayo pia fedha hizo zitatumika kuimarisha huduma za mama na mtoto pamoja na uendeshaji wa vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi vipatavyo 6214".

Kwa upande wake Mratibu wa Kamati ya washirika wa maendeleo wa mfuko wa Afya wa pamoja kutoka ubalozi wa Uswiss, Bi. Jacqueline Matoro ameipongeza serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya kwa kuhakikisha inaimarisha huduma za Afya na upatikanaji wake kuanzia ngazi ya msingi na kuishikuru Wizara ya Afya kwa ushirikiao inaoutoa kwa wadau wa maendeleo katika sekta ya Afya.

Mfuko wa Afya wa pamoja ulianzishwa mwaka 1999 ambapo hadi sasa umeendelea kuunga mkono juhudi za serikali ambapo wadau hao ni Serikali ya Canada, Switzerland, Ireland, World Bank, UNICEF, UNFPA, KOICA, Danida Investment pamoja na mdau mpya Serikali ya Uingereza.

# Hospitali za Rufaa za Mikoa zinazoziba Meno watu wengi kuliko kung'oa

## JULAI 2024




Hospitali za Rufaa za Mikoa zinazotoa huduma ya kuziba Meno watu wengi bila kung'oa

Hospitali za Rufaa za Mikoa zinazoziba watu meno ila bado zinang'oa pia watu wengi

NB:Serikali inaendelea kuboresha Huduma za Kuziba meno bila kung'oa ili huduma hizo kufikia katika Hospitali zote nchini




Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
WIZARA YA AFYA, TANZANIA, TOLEO LA MWEZI JULAI, 2024